TAARIFA KWA AJILI YA WEBSITE YA JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM 2018

PAROKIA YA MT. YOHANE PAULO II, MBEZI MSHIKAMANO

Paroko: Pd. Bartholomew Mrosso 0682 888168, 0743 858826

Shirika: Wamisionari wa Afrika (M.Afr.)

Kanisa la Parokia linaloendelea kujengwa

HISTORIA YA PAROKIA YA MT. YOHANE PAULO II, MBEZI MSHIKAMANO

1. Utangulizi

Parokia ya Mt. Yohane Paulo II, Mbezi Mshikamano ilizinduliwa tarehe 1 Mei 2016. Awali ilikuwa Parokia Teule mwezi Septemba 2015 na kutangazwa Parokia kamili mwezi Aprili 2016. Historia ya Parokia inaanza mwaka 2005 ilipoundwa Kanda ya Mshikamano chini ya Parokia ya Mt. Peter Claver, Mbezi Louis. Wakati huo Kanda ilikuwa na Jumuiya Ndogo ndogo 5. Tarehe 15 Agosti 2009, Baba Paroko wa wakati huo, Pd. Vivian Menezes aliadhimisha misa ya Kanda iliyofanyika eneo la kiwanja kilichonunuliwa na kutangaza kuanzisha Kanda mpya ya Kristo Mfalme, Mshikamano kwa kuunganisha Kanda ya Mshikamano na Kanda ya Victoria iliyokuwa na Jumuiya 3 hivyo Kanda mpya kuwa na Jumuiya 8.

Mwezi Mei 2010 Kanda ya Kristo Mfalme iliongezewa Jumuiya 2 kutoka Kigango cha Bikira Maria wa Mateso, Msakuzi na kuundwa Kanisa Dogo la Kristo Mfalme, Mshikamano likiwa na jumla ya Jumuiya 10. Mwanzoni mwa mwaka 2011 baadhi ya Jumuiya ziligawanywa na kuunda jumuiya 3 mpya na kufanya jumla ya jumuiya 13. Katika kuadhimisha sikukuu ya Somo wa Kanisa Dogo, Sherehe ya Kristo Mfalme tarehe 20 Novemba 2011, Kanisa Dogo lilitangazwa rasmi kuwa Kigango kikiwa na Jumuiya 13 na kupewa somo mpya Mt. Theresia wa Avila. Mwaka 2012 Jumuiya nyingine 4 mpya ziliundwa na kufanya Kigango kufikisha jumuiya 17. Kutokana na jiografia ya eneo la Kigango, mwezi Mei 2014 Jumuiya moja kutoka Parokia ya Makabe ilihamishiwa katika Kigango na kufikisha Jumuiya 18.

Ndani ya eneo la Kigango (sasa Parokia) kuna Nyumba ya Malezi ya Shirika la Wamisionari wa Afrika ambayo ilizinduliwa na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo tarehe 26.11.2009 na kuomba Shirika litoe pia huduma kwa majirani. Mazungumzo yalifanyika kwa kuhusisha uongozi wa Parokia ya Mbezi Louis wakati huo na uongozi wa Shirika, na kuruhusiwa kusali misa moja kwa mwezi katika Nyumba hiyo kuanzia tarehe 29.11.2009. Waamini waliendelea kusali katika Nyumba hiyo na kuongezewa idadi ya misa hadi kuwa na misa kila Jumapili pamoja na shughuli nyingine za kanisa na maandalizi ya ujenzi wa Kanisa la Kigango mpaka tarehe 6 Julai 2014 misa na shughuli nyingine zilipohamia katika eneo la Kanisa la Kigango.

Mnamo mwezi Septemba 2015 Kigango kilipewa hadhi ya kuwa Parokia Teule chini ya usimamizi wa Shirika la Wamisionari wa Afrika ikiwa na vigango vya Msakuzi na Mpiji Magohe. Kutokana na kuwa na jina la somo mmoja na Parokia jirani ya Kibwegere, Mt. Theresia wa Avila, mwezi Desemba 2015 waamini wa Parokia Teule waliomba kubadili somo wake kuwa Mt. Yohane Paulo II. Baba Kardinali alizitangaza Parokia Teule za Mshikamano na Msakuzi kuwa Parokia kamili tarehe 26.04.2016 pamoja na Parokia nyingine nne. Misa ya uzinduzi wa Parokia ilifanyika Dominika ya tarehe 1 Mei 2016, Sikukuu ya Mt. Joseph, somo wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam na kuongozwa na Paroko wa kwanza, Padre Bartholomew Mrosso pamoja na Mkuu wa Shirika la Wamisionari wa Afrika kanda ya Afrika Mashariki (Provincial), Padre Charles Obanya.

Mpaka kufikia mwezi Mei 2017 Parokia ilikuwa na Jumuiya 25 zinazounda Kanda tano (5) zenye Jumuiya tano kila moja.

2. Halmashauri ya Walei Parokia

Halmashauri ya Walei Parokia inaundwa na viongozi wa Kamati Tendaji za Kanda, wenyeviti wa Vyama vya Kitume ngazi ya Parokia pamoja na Kamati Tendaji ya Parokia. Kamati Tendaji ya Parokia ilichaguliwa tarehe 10 Julai 2016 kwa usimamizi wa Uongozi wa Jimbo, na kuapishwa katika ibada ya misa takatifu Dominika ya tarehe 17 Julai 2016. Viongozi hao ni:

Mwenyekiti:	Theophil Mfala
Makamu Mwenyekiti:	Christina Kwayu
Katibu:	Silvani Mng'anya
Katibu Msaidizi:	Antoinette Moshi
Mhazini:	Adam Kamanda
Mhazini Msaidizi	Eva Mushi

3. Eneo na Ujenzi wa Kanisa

Eneo la Kanisa lilinunuliwa kwa michango ya waamini kwa awamu tofauti chini ya uongozi wa Paroko wa Mt. Peter Claver Mbezi Louis mwezi Aprili 2006, na baadaye Paroko wa Mshikamano 2016/17. Ramani ya kanisa iliandaliwa na wataalamu wa ndani katikati ya mwaka 2010 na maandalizi na taratibu za ujenzi wa Kanisa zilifanyika ikiwa ni pamoja na michango ya ujenzi kupitia harambee za kijumuiya za kila mwezi na pia harambee za kifamilia. Ujenzi wa jengo la Kanisa ulianza rasmi tarehe 22 Agosti 2011. Jiwe la msingi liliwekwa tarehe 10 Septemba 2011 na Mhashamu Baba Askofu Salutaris Libena wakati huo akiwa Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam. Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo alitembelea maendeleo ya ujenzi tarehe 16.12.2012 na baadaye Askofu Msaidizi, Mhashamu Askofu Titus Mdoe tarehe tarehe 15.12.2013.

Jengo la Kanisa lina sehemu ya chini (sub-basement) ikiwa na ofisi na ukumbi wenye uwezo wa kuchukua watu wapatao 600 na Kanisa (sehemu ya juu) lina uwezo wa kuchukua waamini 1000 walioketi. Baada ya kufunika sehemu ya chini (sakafu ya Kanisa) mwezi Mei 2014, sehemu hiyo ilianza kutumia kwa ibada za Misa Takatifu Dominika ya tarehe 6 Julai 2014. Parokia pia ilinunua na kukarabati jengo ambalo ni nyumba ya mapadre kwa sasa.

4. Vyama vya Kitume

Parokia kwa sasa ina vyama vya Kitume kumi (10) pamoja na Shirika la Kipapa la Utoto Mtakatifu. Vyama hivyo ni Utume wa Wanaume Katoliki (UWAKA), Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) ambao pia wanawalea Utoto Mtakatifu, Vijana Wafanyakazi Wakatoliki (VIWAWA), Shirikisho la Kwaya Parokia (SHIKWAKA Parokia), Ushirika wa Moyo Mtakatifu wa Yesu, Mt. Vincent wa Paulo, Shirika la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, Utume wa Wanataaluma Wakristo Tanzania (Christian Professionals of Tanzania –CPT), Karismatiki Katoliki, na Utume wa Familia katika Kristo (Couples For Christ – CFC).